

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

08/10/2018

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA AONGEZA MUDA WA KUPIGA MZIKI MATAMASHA YA USIKU.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo ametangaza kuondoa muda wa Kikomo kwa wasanii kupiga mziki kwenye matamasha hadi Saa sita usiku Na sasa amewaongezea muda hadi Saa nane usiku kwa siku za weekend pekee.

Hatua hiyo imepokelewa kwa shangwe na wasanii nchini ambao kilio chao kilikuwa kuongezewa muda wa kufanya matamasha ili waweze kujipatia kipato cha kujikimu kimaisha kuendana na kaulimbiu ya Rais wao Mpendwa Dkt. John Magufuli inayowataka watu kufanya kazi.

Hii pia ni matokeo ya kuimarika kwa ulinzi na usalama wa jiji hilo la kibiashara na ongezeko la Kumbi nyingi zinazozuia kelele kutoka nje (soundproof) ambapo lengo la RC Makonda ni kuona siku moja watu wanafanya shughuli za kibiashara kwa Saa 24.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM